



**KISWAHILI KIDATO CHA PILI  
KAZI YA ZIADA-LIKIZO YA APRILI  
MUHULA WA KWANZA - 2024**

(a) Badilisha sentensi ifuatayo iwe mazoea kwa kutumia kirejeshi “O”

Mtoto anayelia huchapwa

(b) Andika kinyume

Wavulana watatu wanaingia darasani kwa haraka.

(c) Andika sentensi tatu ambazo zaweza kuwa sahihisho la sentensi hii:-

Kule ndimo alipoingia

(d) Taja aina za vitenzi vilivyopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo

Mama amewahi kupika jikoni

(e) Eleza maana ya misemo ifuatayo :-

(i) Giza la ukata...

(ii) Meza mate machungu

(f) Unda vitenzi kutokana na :-

(i) Mkufunzi

(ii) Maeneo

(g) Kwa kutoa mfano mmoja mmoja, taja aina za sentensi za kiswahili

(h) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia vishale

Mwalimu huyu mzuri anafundisha darasani.

(i) Eleza maana mbili za sentensi :-

Mama alimlimia mwanawe shamba

(j) Akifisha sentensi ifuatayo:-

ah huu ndio upuuzi aliotuitia mmoja wao akaropoka.

(k) Tunga sentensi itakayodhihirisha matumizi ya kielezi cha namna mfanano

(l) Andika sentensi ifuatayo katika msemu halisi :-

Mshtakiwa alidai kwamba alikuwa ameonewa kwa kuwa hakuwa ameshiriki ulevi kutoka mwaka uliokuwa umetangulia.

(m) Pambanua viungo vya kisarufi katika kitenzi kifuatacho

Tuliwalimia

(n) Andika upya sentensi ifuatayo kwa kufuata maagizo:

Mizizi ya mibaruti hii iliwaponya watu ambao walikuwa na shida kama hii yenu (kanusha kwa umoja)

(o) Tunga sentensi ukitumia neno “Vile” kama:

(i) Kiwakilishi

(ii) Kivumishi

(iii) Kielezi

(p) Bainisha matumizi viambishi “ku” na “Ji” katika sentensi zifuatazo:-

(i) Mwanafunzi hukusoma kwa bidii

(ii) Atakupiga

(iii) Amejikata

(iv) Mchezaji huyu ni hodari

(q) Andika sentensi ifuatayo kwa ukubwa huku ukikanusha

Kijibwa changu ni kikali sana

2. (a) Jaza mapengo:-

Kutenda Kutendesha

(i) Chota

(ii) Lewa

(b) Taja sauti moja ya;

(i) King’ong’o

(ii) Kiyeyusho

(c) Tumia neno “shujaa” katika sentensi kama:

(i) Kivumishi

(ii) Kielezi...

